# MAKAMBAKO YETU

*www.makambakotc.go.tz* |*Kitengo cha Mawasiliano Serikalini* | *Jarida Maalumu La miaka 11 ya H/M Makambako*

# MIAKA 11 YA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO




#Kwa pamoja tuijenge

# UTANGULIZI

Mchakato wa uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji Makambako

Halmashauri ya Mji Makambako ilianza rasmi mnamo mwezi Julai 1,2012 baada ya kupandishwa hadhi kutoka kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo Makambako hadi kuwa Halmashauri ya Mji,ikiwa ni baada ya Madiwani nane ambao walikuwa wanaziwakilisha Kata nane za Makambako ,kwenye baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakiongozwa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Njombe Kaskazini Mhe.Jackson Mvangila Makweta na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Njombe, Mhe. Deo Sanga(MB).

Madiwani walioshiriki kwenye mabadiliko ya uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji Makambako ni diwani wa Kata ya Kitandililo ambaye kwa sasa ni marehemu, Mhe. John Mwandoloma,Mhe. Hanana Chesco Mfikwa aliyekuwa diwani wa Kata ya Ubena, Mhe. Alimwimike Sahwi, aliyekuwa diwani wa Kata ya Mjimwema, Mhe. Justin Nusulupila Sanga aliyekuwa diwani wa Kata ya Mwembetogwa, Mhe. Richard Chagavalye (Redio) aliyekuwa diwani Kata ya Mahongole ambaye kwa sasa ni marehemu, Mhe. Malla Mgeni aliyekuwa diwani wa kata ya Mlowa, Mhe. Erasto Ngota aliyekuwa Diwani wa Kata ya Utengule na Mhe. Salum Mlumbe, diwani wa Kata ya Lyamkena,Madiwani wote nane ni kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

Mchakato wa uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji Makambako ulianzishwa mwaka 2010 ikiwa ni baada ya mchakato ulioanzishwa mwaka 2005 uliokuwa na lengo la kupata Halmashauri ya Mji kushindikana na badala yake ikaanzishwa Mamlaka ya Mji Mdogo Makambako.Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 mapendekezo ya kuanzisha Halmashauri ya Mji Makambako yaliwasilishwa tena na Waheshimiwa madiwani wakiongozwa na Mbunge wa Jimbo la Njombe Kaskazini kwenye baraza la Madiwani la Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Baada ya Serikali kuu kuridhia kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji Makambako, uchaguzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako kwa mara ya kwanza ulifanyika mwaka 2012 ambapo Mhe. Hanana Chesco Mfikwa, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Ubena alichaguliwa na waheshimiwa Madiwani kutoka Kata nane (8) za Makambako kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Halmashauri ya Mji Makambako na Makamu mwenyekiti aliyechaguliwa alikuwa Mhe.Malla Mgeni- aliyekuwa diwani wa Kata ya Mlowa na Mkurugenzi wa kwanza wa Halmashauri ya Mji Makambako aliyeteuliwa alikuwa ni Bi.Tina Sekambo.

Mchakato wa kubadili Vijiji kuwa Mitaa na kuongeza Idadi ya Kata

Mwaka 2013 mapendekezo ya kubadili vijiji kuwa Mitaa na kuongeza Kata kutoka Kata nane (8) hadi Kata kumi na mbili (12) yalitolewa na kamati za maendeleo za Mitaa/Vijiji pamoja na Kata, kisha kupelekwa kwenye baraza la madiwani la Halmashauri ambapo baadae mapendekezo yaliwasilishwa Ofisi ya Raisi -TAMISEMI ,mwaka 2014 yaliridhiwa na Mitaa 14 ilianzishwa na kuongeza Kata (4) na hivyo kufanya kuwa na jumla ya kata kumi na mbili ambazo zipo hadi sasa.

Kata zilizoongezwa ni Kata ya Kitisi na Kivavi zilizomegwa kutoka kwenye Kata ya Mjimwema, Kata ya Maguvani iliyotoka kwenye Kata ya Ubena, Kata ya Majengo iliyotoka kwenye Kata ya Mwembetogwa. Aidha, Jina la Kata ya Ubena lilibadilishwa na kuitwa Kata ya Makambako kwa ajili ya kuenzi asili ya jina la Makambako kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

JARIDA MIAKA 11.indd 2 7/11/2023 5:26:50 AM

## VIONGOZI WA MAMLAKA YA MJI MDOGO HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



**Mhe. Deo Kasenyenda Sanga,Mbunge wa jimbo la Makambako.**



**Mhe. Hanana C. Mfikwa Mwenyekiti wa H/M Makambako tangu 2012 hadi sasa.**



**Bw. Godwin Benne,aliyekuwa Mkurugenzi wa Mji Mdogo Makambako kabla ya kuwa H/M Makambako.**




**Bi. Tina Sekambo,aliyekuwa Mkurugenzi wa H/M Makambako 2012 - 2014**



**Bi. Vumilia Nyamoga ,aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako Mwaka 2015 -2016**



**Bw. Paulo S. Malala,aliyekuwa Mkurugenzi wa H/M Makambako mwaka 2016 hadi 2021**



**Bw. Kenneth K. Haule Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako kuanzia 2021 hadi sasa.**

## Baadhi ya Madiwani waliokuwepo kabla ya Halmashauri ya Mji Makambako kupandishwa hadhi



Mhe. Malla Mgeni



Hayati Mhe. John Mwandoloma



Mhe. Justin Nusulupila Sanga



Mhe. Alimwimike Sahwi



Mhe. Salum Mlumbe

# HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA NA HALI YA MIUNDOMBINU KISEKTA KABLA NA BAADA YA KUANZISHWA KWA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO MWAKA 1.7.2012



## Sekta ya Barabara

### TARURA

Halmashauri ya Mji Makambako ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 667.97 .

Katika kipindi cha Mamlaka ya Mji Mdogo ,Makambako haikuwa na barabara za lami kwenye Mitaa kama ilivyo sasa. Barabara za Lami zilizokuwepo ilikuwa ni barabara ya Makambako - Songea, barabara ya Makambako – Mbeya na barabara ya Makambako – Iringa. Aidha, barabara zote za mitaa na Vijiji kwa wakati huo zilikuwa ni za vumbi na ambazo hazipitiki kwa urahisi kwa nyakati zote.

Baada ya kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji , Makambako ina barabara za lami kilomita 16.72 katika mitaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na barabara ya Posta – Mizani ,barabara ya njia panda ya misheni hadi soko la nyanya,barabara ya polisi-kituo cha afya, barabara ya A- One Lodge – DS Hotel ujenzi unaendelea barabara ya Mlando – kanisa la wasabato ,barabara ya Mwigune-Mchape,barabara ya Lumumba(stoo za samaki),barabara ya Mitumbani na TRA na barabara ya stendi.

Vilevile, ujenzi wa madaraja, makavati na uboreshaji wa barabara za vijijini umefanyika na utaendelea kufanyika kwa kadri ya mahitaji.



Baadhi ya barabara za Mitaa za kiwango cha lami katika Halmashauri ya Mji Makambako.



## Sekta ya Maji

### Maji Mjini

Huduma ya maji Mjini inatolewa nakusimamiwa na Mamlaka ya MajiSafi Makambako(MAKUWASA) inayohudumia Kata 9 zilizopo Mjini, Kata ya Mjimwema, Kitisi, Lyamkena, Kivavi, Maguvani, Mwembetogwa, Makambako, Majengo na  Mlowa.

Katika kipindi cha miaka ya nyuma kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji Makambako tatizo la maji lilikuwa kubwa mitaa mbalimbali ,ambapo maji yalitolewa kwa mgao hasa nyakati za kiangazi na kuwalazimu wananchi kutumia muda mwingi kutafuta maji na shughuli za kiuchumi kusimama.

Kwa sasa Halmashauri ya Mji Makambako ina jumla ya  wakazi  117,743 kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022,waliopo katika eneo la huduma na wakazi wanaopata huduma ya majisafi ni 77,239 ambayo ni sawa na 65.6% .

Mahitaji ya Maji kwa siku katika Mji wa Makambako ni lita millioni 10,860 na uwezo wa uzalishaji hadi Aprili mwaka huu  ni lita milioni 4,686 kwa siku sawa na 43.15% ya mahitaji yote na Vyanzo vya maji  vinavyotumika ni Maji ya Mtiririko (FUKULWA-Mtwango) na Visima virefu 12 vilivyopo hapa Mjini ambavyo vimesaidia kuongeza masaa ya upatikanaji wa Huduma ya maji ya uhakika , kutoka masaa 16 hadi 21 kwa siku na kuondoa mgao wa maji.

Serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maji ili kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu kwa wananchi.



Foleni ya wananchi wakisubiri huduma ya maji katika moja ya kituo kutokana na changamoto ya ukosefu wa maji ambapo kwa sasa hakuna foleni kutokana na jitihada za Serikali za kuhakikisha wananchi wanapata maji.



Mradi wa Maji Mahongole - Usetule

### Maji Vijijini

**H**uduma ya maji vijijini inatolewa na kusimamiwa na Wakala wa maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na vyombo vya kutoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWS0s) katika Kata ya Mahongole,Kitandililo na Utengule.

Kabla ya miradi hii, Vijiji vya Usetule, Mahongole, Mtulingala, Nyamande, Mbugani, Ibatu na Ikelu vilikuwa vinategemea huduma ya maji kupitia visima vya mkono na vijito vilivyopo kwenye vijiji hivyo ambavyo si salama kwa afya ya binadamu.

Hata hivyo kipindi cha kiangazi maji hayo yalikuwa yanakauka hivyo kufanya wananchi kuhangaika kutafuta huduma ya maji mbali na makazi yao, ambapo muda mwingi ulipotea na kusababisha kuathirika kiuchumi.

Miradi ya maji imetekelezwa kwenye Kata hizo inahudumia wakazi wapatao 18,230 katika Kijiji cha Ikelu,Mtulingala,Mbugani,Nyamande,Ibatu,Usetule na Mahongole.


Mradi wa Maji Mtiririko Mahongole-Usetule




Kituo cha Afya Makambako

## Sekta ya Afya

Katika kipindi cha Mamlaka ya Mji Mdogo, Makambako kulikuwa na Kituo kimoja cha Afya cha Makambako, Zahanati zilikuwa nne (4) ambazo ni Zahanati ya Roman Catholic (RC) Makambako, Manga, Kifumbe na Kitandililo.

Baada ya Kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji MakAmabako,ujenzi wa maabara na wodi la Mama na Mtoto na jengo la upasuaji katika kituo cha Afya Makambako ulifanyika ili kutoa huduma zote za Afya kwa Wananchi wa Makambako na maeneo jirani na kuwapunguzia mwendo wa kufuata huduma za upasuaji Hospitali ya Ilembula,Ikonda na Hospitali zingine.

Aidha, ili kupunguza msongamano katika Kituo cha Afya Makambako,ujenzi wa Kituo cha Afya Lyamkena ulianzishwa na sasa Kituo hicho kimekamilika na huduma zinatolewa.

Pia,Ujenzi wa Zahanati ya Maguvani, Zahanati ya Ibatu, Zahanati ya Mtanga, Zahanati ya Ngamanga-,Zahanati ya Ikwete,Zahanati ya Utengule,Zahanati ya Usetule,Ujenzi wa Zahanati ya Mahongole,Zahanati ya Mkolango,Zahanati ya Majengo na Zahanati ya Kitisi ulianzishwa na kwa sasa baadhi ya Zahanati hizo zimeanza kutoa huduma na nyingine zipo katika hatua za ukamilishaji.

Pia,kwa sasa Halmashauri ya Mji Makambako ina jumla ya vituo 13 vya kutolea huduma za Afya,Hospitali ya Mji 1 iliyopo Mlowa,Vituo vya Afya 3 kati ya hivyo vituo viwili vinatoa huduma na kituo kimoja cha Kitandililo kipo hatua za ukamilishaji na Zahanati 10 za Serikali.



**Baadhi ya Majengo katika Hospitali ya Mji -Mlowa**




**Jengo la wagonjwa wa dharura- Hospitali ya Mji Mlowa**



## Sekta ya Elimu

Elimu Msingi

Wakati wa Mamlaka ya Mji Mdogo Makambako inaanzishwa, kulikuwepo na shule za msingi (09) ambazo ni; Ikwete, Uhuru, Mludza, Mlowa, Makambako, Idofi,Lyamkena,Kiumba na shule ya Msingi Azimio ambazo zote zilijengwa na Serikali kwa kushirikiana na wananchi.

Aidha,kutokana na ongezeko la wanafunzi, jitihada mbalimbali za kuongeza ujenzi wa shule nyingine mpya zilifanyika kwa kuanza na ujenzi wa Shule ya Msingi Mshikamao ,ujenzi wa shule ya Msingi Mwembetogwa ,ujenzi wa shule ya msingi Kahawa na shule ya Msingi maendeleo.





**Baadhi ya Madarasa,S/M Magongo**

Kwa sasa Halmashauri ya Mji Makambako ina shule za msingi 55,48 za Serikali na shule 7 za binafsi.Aidha,Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya shule na nyumba za walimu.



Jengo la shule ya kwanza ya Msingi ambayo kwa sasa ni shule ya Msingi Makambako



Nyumba ya zamani ya Mwalimu S/M Mfumbi



Nyumba ya sasa ya walimu (2 in 1) s/m Mfumbi




Shule ya sekondari MakambakoB

## Elimu Sekondari

Kabla na baada ya kuanzishwa Mamlaka ya Mji Mdogo Makambako, kulikuwa na shule moja ya Sekondari ,ambayo ni shule ya Sekondari Makambako iliyokuwa inamilikiwa na Jumuiya ya Wazazi Njombe(NDDT – Njombe District Development Trust) iliyosajiliwa mwaka 1984.

Baada ya miaka kadhaa Shule hiyo ilibadilishwa na kuwa ya Serikali,na zikaanzishwa shule nyingine za Sekondari ili Kupunguza Msongamano wa wanafunzi ambapo shule ya Maguvani ilianzishwa na kuanza rasmi mwaka 2005,baada ya kufanikisha kujenga shule ya Sekondari Maguvani Halmashauri iliendelea na ujenzi wa shule zingine.

Hivyo,kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji Makambako Mwaka 2012,kulikuwa na shule za sekondari 7 za Serikali ambazo ni Makambako,Maguvani,Kipagamo,Mukilima,Mtimbwe,Lyamkena na Mahongole,shule binafsi 4 ambazo ni MCF Makambako,Emmaberg,Genesis na Naboti sekondari.



Moja kati ya Maabara ya kisasa katika shule za Sekondari

Baada ya kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji Makambako,kuna jumla ya shule za Sekondari 17 ,za Serikali ni 12 na 5 ni binafsi na shule ya sekondari Makambako ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

Shule za Serikali zilizoanzishwa baada ya Mwaka 2012 ni Deosanga,Kitandililo,Mlowa,Mlumbe na Kitisi sekondari na shule binafsi ya Kerith Brook.



Shule ya Sekondari Kitisi




Sekta ya Nishati – TANESCO

Uunganishaji wa umeme kupitia mradi wa REA umefanyika kwa kiwango cha kuridhisha ambapo vijiji 22 katika wilaya ya ki-TANESCO Makambako vimeunganishiwa umeme Sawa na asilimia 82 ya vijiji 27 vilivyotarajiwa kuunganishiwa umeme.

Upatikanaji wa umeme kwenye vijiji hivi vimeongeza hali ya ukuaji wa uchumi kwa wananchi kwakuwa wananchi wanaweza kujikita kwenye shughuli za uzalishaji kwa kuanzisha viwanda vidogovidogo,kuboresha mazingira na kukuza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja.

Pia,TANESCO imefanikiwa kuwasha umeme kwenye Kata zote 12, vijiji 14 na mitaa 32 kati ya 54 za Mji wa Makambako kupitia wakala wa umeme vijijini yaani REA na TANESCO, na mpango uliopo ni kuhakikisha mitaa/vitongoji vyote vinapata huduma ya umeme.



Zoezi la uunganishaji wa Umeme wa REA katika Kijiji cha Ikelu

## Sekta ya Utawala

Jengo la utawala la Mamlaka ya Mji Mdogo Makambako



Jengo la utawala la Halmashauri ya Mji Makambako



## MATUKIO KATIKA PICHA




Nyumba pacha ya Walimu shule ya Msingi Mfumbi.



Madarasa mawili na ofisi moja,katika shule ya msingi kongwe ya Mawande.



Zahanati ya Maguvani.



Zahanati ya Ikelu imejingwa kupitia TASAF.




Moja kati ya Vikundi vya vijana ambao wamenufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri kwa Vikundi vya Wanawake,Vijana na watu wenye Ulemavu.




Gari la Miradi ya maendeleo la Halmashauri ya Mji Makambako lililonunuliwa kwa fedha za Mapato ya ndani.

## BARAZA LA MADIWANI 2020-2025



**Mhe. Hanana Mfikwa**
**Diwani -Kata ya Maguvani**
**(Mwenyekiti - Halmashauri)**



**Mhe. Rosemary Lwiva**
**Diwani - Kata ya Majengo**
**(Makamu Mwenyekiti -Halmashauri**



Kutoka Kushoto: Mhe. Mario Kihombo,diwani wa Kata ya Mahongole na kulia ni Mhe. Salum Mlumbe- diwani wa Kata ya Lyamkena.



Kutoka Kushoto:Diwani wa Kata ya Makambako,Mhe. John Ngimbudzi,Mhe. Oddo Chaula,diwani wa Kata ya Mwembetogwa na Mhe. Stepano Mgoba, diwani wa Kata ya Utengule.



Kutoka Kushoto:
Mhe. Flora Nyaluke,diwani viti maalumu Kata ya Mjimwema na Mhe. Angelina Kimbawala, diwani viti maalumu Kata ya



Wa kwanza kushoto:Mhe. Alimwimike Sahwi,diwani wa Kata ya Kivavi na diwani wa Kata ya Mlowa,Mhe. Odillo Fute.



Kutoka kushoto: Mhe. Stella Uhemba,diwani viti maalumu Kata ya Lyamkena na Mhe. Lucy Mbogela ,diwani viti maalumu Kata ya Mwembetogwa.




Kutoka kushoto: Mhe. Imani Fute,diwani wa Kata ya Kitandililo na Mhe. Nolasko Mlowe,diwani wa Kata ya Mjimwema.



Mhe. Navy Sanga,diwani wa Kata ya Kitisi.

# RAMANI YA MIPAKA YA UTAWALA YA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO




**HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

> **makambakotc**

> **makambakotc**

> **www.makambakotc.go.tz**

> **makambakotc**

**Jarida hili limeandaliwa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Halmashauri ya Mji Makambako**
**S.L.P 405**
**MAKAMBAKO**